# MAMBO YA HAKIKA

**"Watoto milioni mbili wanalelewa na wazazi wa LGBT."**

***-Mradi wa Maendeleo ya Harakati na Baraza la Usawa la Familia na Kituo cha Maendeleo ya Marekani***

**"19% ya watu waliobadilisha jinsia wamekatazwa kukodisha na 11% wamefukuzwa kwa sababu ya kitambulisho chao cha kijinsia."**

***-Kituo cha Kitaifa cha Usawa wa Waliobadilisha Jinsia***



**"48% ya wenzi wa jinsia moja ambao walipiga simu kwenye vituo vya kuishi vya wazee walipatwa na dhuluma mbaya tofauti kutoka kukatazwa kukodisha hadi kupewa huduma chache."**

*-Kituo cha Utafiti wa Kitaifa juu ya Uzeekaji wa LGBT*

**"Mtu 1 kati ya 3 wa LGBT ni mtu wa rangi. Watu wa rangi wa LGBT wana machaguo machache ya makazi ambayo yanaweza kuwasukuma katika makazi yasiyostahili au mitaa ya gharama kubwa."**

*-Mradi wa Maendeleo ya Harakati na Kituo cha Maendeleo ya Amerika*

**"Wenzi wa jinsia tofauti walipendelewa zaidi kuliko wenzi wa jinsia moja wa kiume katika asilimia 15.9 ya majaribio, na zaidi ya wenzi wa jinsia moja wa kike katika asilimia 15.6."**

*-Idara ya Marekani ya Makazi na Maendeleo ya Mjini*

# RASILIMALI

EQUAL HOUSING OPPORTUNITY

Ikiwa unafikiria kwamba umebaguliwa katika shughuli ya kupata makazi, wasiliana na:

Ushirikiano wa Usawa wa Makazi wa Northwest
35 W. Main Ave, Suite 250
Spokane, WA 99201

509-325-2665
1-800-200-FAIR (3247)
Faksi: 1-866-376-6308
www.nwfairhouse.org

NWFHA inaweza kukushauri juu ya machaguo yako na kukutetea. Huduma za NWFHA ni za bure.

# RASILIMALI MTANDAONI

**Tume ya Haki za Kibinadamu ya Jimbo la WA**
www.hum.wa.gov

**Kampeni ya Haki za Binadamu**
www.hrc.org

**Kituo cha Kitaifa cha Usawa wa Waliobadilisha Jinsia**
www.transequality.org

**Kikosi cha Kitaifa cha LGBT**
www.thetaskforce.org

**SAGE (Huduma na Utetezi kwa wazee wa LGBT)**
www.sageusa.org

Kazi ambayo ilitoa msingi wa chapisho hili iliungwa mkono kwa sehemu na ufadhili chini ya ruzuku kutoka Idara ya Makazi na Maendeleo ya Mjini ya Marekani. NWFHA inawajibika kikamilifu kwa taarifa na tafsiri zilizomo katika chapisho hili. 4/16 NWFHA

# LGBT
## Haki za Usawa wa Makazi



## Vidokezi vya Haraka vya Kukodisha na Umiliki wa Nyumba

*"...kuna ushahidi…kwamba wasagaji, shoga, watu wanaopenda jinsia zote mbili na watu waliobadilisha jinsia na familia zao wanatengwa kiholela kutoka kwa baadhi ya fursa za makazi katika sekta ya kibinafsi."*

***~Idara ya Marekani ya Makazi na Maendeleo ya Mjini***

**USHIRIKIANO WA USAWA WA MAKAZI WA NORTHWEST**


(509) 325-2665
1 (800) 200-FAIR (3247)
www.nwfairhouse.org

# Vidokezi vya Haraka: Kukodisha kwa Watu Binafsi wa LGBT na Familia

Chagua nyumba ya kukodisha unayopenda ambayo inafaa bajeti yako ya kifedha; sio lazima ujichague kutoka kwa eneo Fulani kwa sababu ya mwelekeo wako wa kimapenzi au kitambulisho cha kijinsia.

Katika jimbo la Washington, una haki ya kufichua hadharani utambulisho wako wa LGBT. Ni haramu kwa mtu kukubagua kwa makazi.

Ukiwa na kitambulisho cha kijinsia, una haki ya kufichua jina na/au kiwakilishi nafsi unayopendelea (yaani*yeye, wao...*) **Dokezo: Kwa nyaraka za kisheria,unaweza kuhitaji kutoa kitambulisho cha kisheria. Hata hivyo, unaweza kutaja jina na kiwakilishi nafsi ambayo ungependa kuitwa nje ya mahitaji ya nyaraka zako za kisheria. Ikiwa nyaraka zako za kitambulisho zitabadilika, unaweza kutoa nyaraka zako za kisheria za hivi karibuni.*



Ukipatwa na unyanyasaji wa mpangaji kwa mpangaji, (yaani kutusiwa,uharibifu wa mali, n.k.) kulingana na mwelekeo wako wa kimapenzi au kitambulisho chako cha kijinsia,weka malalamiko yako kwa maandishi kwa usimamizi au mmiliki wa nyumba ya kukodisha. Ikiwa unyanyasaji hautakoma, wasiliana na wakala wa usawa wa makazi wa eneo lako na uwasilishe malalamiko ya usawa wa makazi.

Weka nyaraka na nakala zinazohusiana na muamala wako wa kupata makazi kila wakati (yaani matangazo, mikataba ya kukodisha, risiti, notisi na malalamiko).



## Ulinzi wa Makazi ya Serikali ya LGBT

Kwa sasa,hakuna sheria za serikali ambazo zinalinda dhidi ya ubaguzi kulingana na mwelekeo wa kimapenzi.

Walakini, Sheria ya Usawa wa Makazi inajumuisha ulinzi kwa msingi wa jinsia. Kwa hivyo, watu wenye jinsia ambayo haiendani na kanuni, jinsia yenye utata, au waliobadilisha jinsia yao wanaweza kutafuta ulinzi dhidi ya ubaguzi wa makazi chini ya msingi huu.

Kwa kuongezea, Sheria ya Usawa wa Upataji wa Nyumba ya LGBT inayotekelezwa na Idara ya Marekani ya Makazi na Maendeleo ya Mjini inasema kuwa watu wa LGBT hawawezi kukatazwa makazi katika mipango ya serikali inayohusiana na makazi ya bei nafuu (yaani Sehemu ya 8, makazi ya umma, rehani zilizo na bima ya FHA, n.k.)

## Ulinzi wa Jimbo la Washington la LGBT

Mnamo tarehe 8 Juni 2006, Sheria ya Jimbo la Washington Dhidi ya Ubaguzi (WLAD) (RCW 49.60) ilikataza ubaguzi katika makazi kwa msingi wa mwelekeo wa kimapenzi na kitambulisho cha kijinsia.

Sheria hii inakukinga kutokana kwa kukatazwa kukodisha au kuuza au shughuli zingine zinazohusiana na makazi. Ni ubaguzi kwako kutendewa kwa njia tofauti kwa sababu ya mwelekeo wako wa kimapenzi au kitambulisho cha kijinsia kama vile kupewa vifaa vichache,kutozwa ada kwa kupata mwenzi, au kuambiwa kuishi katika jengo fulani, eneo au mtaa, n.k.

# Vidokezi vya Haraka: Umiliki wa nyumba kwa Watu Binafsi wa LGBT na Familia

Fanya utafiti na utembelee benki na wakopeshaji mbalimbali ili ujue aina za mikopo ya nyumba inayopatikana kwa bajeti yako ya kifedha. In Washington state, whether you are partnered or married, lenders need to treat you as equally as partnered or married heterosexual couples while processing your loan application.

Zunguka ukitafuta wakala wa uuzaji wa nyumba. Hakuna wakala wa uuzaji wa nyumba mmoja tu anayefaa mtu mmoja. Ni kama ununuzi wa nguo, saizi moja haitoshi wote. Pata anayekufaa.

Chagua eneo la nyumba ambalo unapenda na unaweza kumudu; usielekezwe kuchagua mahali ambapo "unaweza kujisikia huru zaidi" au "pana watu wengi kama wewe." Una haki ya kuishi mahali popote ambapo sifa zako za ustahili (uwezo wa kupewa mkopo, uwiano wa deni kwa mapato, historia ya ajira, n.k.) zinakidhi mahitaji ya kifedha.

Kuhusiana na unyanyasaji kama mmiliki wa nyumba, piga ripoti na wasilisha malalamishi ya usawa wa makazi kwa HUD.

Zunguka ukitafuta na ufanye utafiti kuhusu chaguo bora kwa bima ya mmiliki wa nyumba. Pia, ikiwa una mwenzi au uko kwenye ndoa nyinyi wawili mnaweza kuwa kwenye sera moja.

